

MKURUGENZI MACHELA AZUNGUMZA NA WENYEVITI WA MITAA MANISPAA YA MOROGORO

Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, ndugu Ally Machela amewataka wenyeviti wa mitaa kushirikiana na Menejimenti ya Manispaa hiyo kuweka utaratibu mzuri wa uzoaji taka na ukusanyaji wa ada ya uzoaji taka ili kuhakikisha mazingira ya Manispaa yanakuwa safi na salama.

Mkurugenzi Machela ametoa rai hiyo wakati akizungumza na wenyeviti wa mitaa yote 294 ya Manispaa ya Morogoro katika kikao kilichofanyika leo tarehe 11.08.2023 kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Manispaa na kuwahimiza wenyeviti hao kuwahamasisha wananchi kuhusu kufanya usafi katika kaya na mitaa yao, kuhakikisha kila kaya inavyo vifaa vya kuhifadhia taka na kuhamasisha wananchi kulipa kwa wakati ada za uzoaji taka, ambayo inatarajiwa kuwa shilingi elfu tatu (3,000) kwa kila kaya.

"Wahabarisheni wananchi kwamba, zoezi la uzoaji taka litakapoanza, kila mji utatakiwa kulipa ada ya taka shilingi elfu tatu kwa mwezi bila kujali kuna familia ngapi ndani ya mji huo na kwa ambaye hatalipa ada hiyo atachukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani na kulipa faini, kwa sababu yeye atakuwa anachangia kudororesha uwezo wa Manispaa kuzoa taka kwa wakati" alieleza Machela.

Vilevile, Mkurugenzi Machela amewataka wenyeviti hao wajue kwamba asilimia saba (7%) ya makusanyo ya ada ya ukusanyaji taka itaingizwa kwenye akaunti zao za mitaa, asilimia tano (3%) itaenda kwenye Kata na asilimia 90 itaenda Manispaa ili kuleta ufanisi katika zoezi hilo mara litakapoanza.

Kwa upande mwingine, Mkurugenzi Machela ametumia kikao hicho kueleza mafanikio ambayo Manispaa ya Morogoro imeweza kuyafikia kwa kipindi cha miaka miwili tangu mwaka wa fedha 2021/2022, katika sekta za Elimu na Afya, kisha akaeleza baadhi ya vipaumbele vya Manispaa kwa Mwaka huu wa Fedha 2023/2024.

"Wakati nilipowasili kwenye Manispaa hii Machi, 2021, kipaumbele changu cha kwanza kilikuwa ni kuboresha sekta za Elimu na Afya na ninamshukuru Mungu kwamba tangu kipindi hicho mpaka sasa hivi, katika sekta ya Elimu tumeweza kujenga shule sita mpya za sekondari na katika sekta ya Afya tumeweza kujenga Zahanati 12 katika Kata mbalimbali na Vituo vya Afya viwili katika Kata za Tungi na Lukobe. Sasa katika mwaka huu wa Fedha kipaumbele namba moja cha bajeti yetu ni kumaliza tatizo la madawati katika shule zote za Msingi na Sekondari. Aidha kipaumbele namba mbili ni kukamilisha maboma ya ofisi zote za Kata na kukarabati zile zilizochakaa. Lakini wakati tunaimarisha Ofisi za Kata tutaona jinsi ya kuimarisha Ofisi za Mitaa pia" alifafanua Machela.

Nao wenyeviti wa mitaa wametoa mapendekezo kuhusu namna bora ya uzoaji taka katika mitaa yao na kuomba kupewa mafunzo ya mara kwa mara kuhusu utekelezaji wa majukumu yao ili wawe na weledi zaidi, mambo ambayo Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, ndugu Ally Machela ameyapokea na kuahidi kuyashughulikia.

Aidha, kikao baina ya wenyeviti wa mitaa na mkurugenzi wa manispaa ya Morogoro kuhusu usafi na mazingira kimehitimishwa kwa mafanikio makubwa ambapo wenyeviti wote

wameridhia kushirikiana kikamilifu na Ofisi ya Mkurugenzi kuhakikisha suala la uzoaji taka mitaani linasimamiwa vyema ili kuifanya Manispaa ya Morogoro kuwa safi na salama.

MWISHO